

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO: DOMINIKA 26 YA MWAKA C - 28.09.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA<br>28.09.2025 | **DOMINIKA YA 26 YA MWAKA C WA KANISA**<br>Mchango wa pili kwa ujenzi |
| 2. | JUMATATU<br>29.09.2025 | Sikukuu ya Wat. Mikaeli, Gabrieli na Rafaeli, Malaika Wakuu |
| 3. | JUMATANO<br>01.10.2025 | Kumbukumbu ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu, Mtawa<br>Kuanza kwa mwezi wa Rozari ya Bikira Maria, kusali saa 11:00 jioni |
| 4. | ALHAMISI<br>02.10.2025 | Kumbukumbu ya Wat. Malaika Walinzi wetu |
| 5. | JUMAMOSI<br>04.10.2025<br><br>JUMAMOSI YA KWANZA YA MWEZI | Kumbukumbu ya Mt. Francis wa Asizi, Mwanzilishi wa Shirika. Kutakuwa na Misa katika Kanda A kuhitimisha matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria, saa 1:00 asubuhi.<br><br>Kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa Kamati Tendaji za Jumuiya za Mt. Augustino na Mt. Bernadeta<br><br>Ni Jumamosi ya kwanza ya mwezi: Misa Parokiani kwa heshima ya Moyo Safi wa Bikira Maria, saa 3:00 asubuhi. |
| 6. | DOMINIKA<br>05.10.2025<br><br>UZINDUZI MAVUNO PAROKIA NA KUAPISHWA VIONGOZI | **DOMINIKA YA 27 YA MWAKA C - *DOMINIKA YA ZAKA***<br><br>**Misa Moja: Saa 2:00 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Perpetua na Mt. Secilia<br>Watangaza Neno: Pius Laswai na Oresta Luambano<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya Miito ya Kitawa, Mapadre. |
| 7. | UANDIKISHAJI MAFUNDISHO YA KOMUNYO NA KIPAIMARA | Uandikishaji wanafunzi wa Komunyo ya kwanza na Kipaimara utahitimishwa Jumamosi ijayo, kuanzia saa 3:00 asubuhi. Komunyo 1 wawe darasa la 3 hadi la 5, umri kuanzia miaka 10. Kipaimara darasa la 5-6, waje na wazazi/walezi na fomu ya huduma kutoka Jumuiya na vyeti vya ubatizo. Mafundisho yataanza Jumamosi 11.10.2025. |
| 8. | KUAPISHWA KWA VIONGOZI WALIOCHAGULIWA KATIKA JUMUIYA | Baba Paroko ameridhia viongozi waliochaguliwa kulingana na taratibu - Vyama vya kitume Jumuiya na Kamati Tendaji za Jumuiya waanze kazi, na wataapishwa rasmi Dominika ijayo 05.10.2025 katika Misa itakayoadhimishwa kuanzia saa 2:00 asubuhi. Jumuiya ambazo hazijakamilisha uchaguzi au kuwasilisha fomu za matokeo ya uchaguzi ziwe zimefanya hivyo mwisho Jumatano 01.10.2025. |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | RATIBA YA MAVUNO PAROKIA 2025 | Baada ya kupata dokezo na mafundisho ya awali kuhusu maana ya mavuno leo tunakumbushwa na Dominika ijayo tutafanya uzinduzi rasmi wa mavuno Parokia katika Misa moja, saa 2:00 asubuhi. Kila familia kuwasilisha malengo ya mavuno ya 2025 kupitia Jumuiya zao.<br>- Kuhitimisha Mavuno Parokia, Dominika ya 02.11.2025 ikijumuisha mnada wa vitu vya mavuno kwa Misa moja saa 2:00 asubuhi. |
| 10. | KAMPENI YA KAPU LA MAMA MARIA KWA RADIO MARIA 2025 | Radio Maria inazindua Kampeni ya Kapu la Mama Maria kwa Dekania za Mbezi Louis, Mavurunza, Kibaha leo 28.09.2025 hapa Parokiani. Kampeni itahusisha kutembeza Sanamu ya Mama Bikira Maria katika familia za Parokia kwa wiki 9 na kuhitimishwa 29.11.2025. Kampeni itaambatana na ugawaji na ukusanyaji wa bahasha na Misa za Kanda kwa heshima ya Mama Maria. Uzinduzi wa matembezi ya sanamu utasindikizwa na mchango wa nia binafsi. Sanamu itakabidhiwa Kanda A kuanza matembezi (*angalia ratiba hapo chini*). Kila Jumamosi matembezi yatahitimishwa kwa Misa katika Kanda na kukabidhiwa Kanda inayofuata. |
| 11. | MWAKA MPYA WA MALEZI – WAMISIONARI WA AFRIKA | Mwaka mpya wa malezi 2025/26 kwa Nyumba ya Malezi ya Wamisionari wa Afrika umezinduliwa jana. Mafrateri 15, watano kutoka kila nchi - Tanzania, Kenya na Uganda wamepangwa kufanya utume katika Jumuiya na Vyama vya Kitume, tuwasaidie. Jumuiya zilizopangiwa mafrateri na hazikufika katika Misa jana viongozi wabaki kukutana nao. Wataanza kusali katika Jumuiya Jumamosi ijayo (*angalia mgawanyo katika JNNK, VMJ)* |
| 12. | WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO | Warsha ya waamini wote wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam itafanyika Jumamosi 29.11.2025 katika viwanja vya Parokia ya Kristo Mfalme Tabata kuanzia saa 2:00 asubuhi. Kutakuwa na Mada mbili,<br>1. Uchaguzi/Uongozi katika Kanisa<br>2. Mwaka wa Jubilei Kuu<br>Kutakuwa pia na vyeti kwa wenye Jubilei za miaka 25, 50 na 75.<br>Ada ya ushiriki ni 5,000/=.<br>*Jumuiya 15 bado hazijachukua fomu na kadi za kuandikisha washiriki.* |
| 13. | TAARIFA YA UTENDAJI KWA KIPINDI CHA UONGOZI | Kamati zinazomaliza kipindi cha uongozi kwa vyama vya Kitume, Jumuiya, Kanda, na Parokia zinakumbushwa kuandaa taarifa fupi kisha kuwasomea wanaowaongoza na kuwasilisha nakala ofisini (*rejea mwongozo uliotolewa*). |
| 14. | CHAKULA KWA WAHITAJI | Chakula kwa wahitaji kitatolewa Jumanne 30.09.2025 saa 10:00 jioni. Wahusika wafike kwa wakati. |
| 15. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini Letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

**MATEMBEZI YA SANAMU YA BIKIRA MARIA KATIKA MWEZI WA MARIA NA KAMPENI YA KAPU LA MAMA 2025**

| WIKI | TAREHE | KANDA HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | 28/09 - 04/10 | A |
| 2 | 04/10 – 11/10 | B |
| 3 | 11/10 – 18/10 | C |
| 4 | 18/10 – 25/10 | D & E |
| 5 | 25/10 – 01/11 | F & G |
| 6 | 01/11 – 08/11 | H |
| 7 | 08/11 – 15/11 | I |
| 8 | 15/11 – 22/11 | J |
| 9 | 22/11 – 29/11 | K |

## MATANGAZO NDOA KWA MARA YA KWANZA

Remigi Reginald Mrema BIN Reginald Ndetola Mrema na Mariana Mtauli Massawe wa Mbezi Mshikamano
Anatarajia kufunga ndoa na:
Lydia Thomas Komu BINTI Thomas Gervas Komu na Rose Daudi Manyanga wa Parokia ya Bikira Maria Madale

## KWA MARA YA PILI

Mauruce Francis Hway BIN Francis Gerald Hway na Agnes Philipo Kessy wa Parokia ya Mbezi Mshikamano
Anatarajia kufunga ndoa na:
Monica John Samwel BINTI John Samwel Mzimba na Neema Robnson Kupatikana wa Parokia ya Mbezi Mshikamano.

## KWA MARA YA TATU

Charles Venance Mgimwa BIN Venance Abdallah Mgimwa na Salome Venance Mgimwa wa Parokia ya Makuburi Dar es Salaam,
Anatarajia kufunga ndoa na:
Lydia David Msabi BINTI David Cleophas Msabi na Elizabeth Msabi wa Parokia ya Vijibweni, Kigamboni
Kaka wa Bibi harusi mtarajiwa ni mwanaparokia ya Mbezi Mshikamano.

**MASOMO DOMINIKA YA 27 YA MWAKA C – 05.10.2025**

| | |
|---|---|
| SOMO I | Hab 1:2-3; 2:2-4 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 95:1-2, 6-9 (K) |
| SOMO II | 2Tim 1:6-8, 13-14 |
| SHANGILIO | Yn 15:15 |
| INJILI | Lk 17: 5-10 |

**Jumuiya 15 ambazo bado hazijachukua fomu na kadi za kuandikisha washiriki warsha ya Waamini wote 29.11.2025.**

1. Mt. Martha
2. Mt. Gaspar del Bufalo
3. Mt. Silvester
4. Mt. Stefano Shahidi
5. Mt. Yuda Thadei
6. Familia Takatifu
7. Mt. Martin de Porres
8. Mt. Joseph Mfanyakazi
9. Mt. Rafaeli Malaika Mkuu
10. Kristo Mfalme
11. Mt. Monika
12. Mt. Paulo Mtume
13. Mt. Antoni wa Padua
14. Mt. Perpetua
15. Mt. Yohane Mbatizaji

**JUMUIYA AMBAZO HAZIJAREJESHA MATOKEO YA UCHAGUZI WA CHAMA CHA KITUME HATA KIMOJA**

1. Mt. Katarina wa Siena
2. Mt. Martha
3. Mt. Yohane Maria Vianney
4. Mt. Silvester
5. Mt. Stefano Shahidi
6. Mt. Yuda Thadei
7. Mt. Martin de Porres
8. Mt. Joseph Mfanyakazi
9. Mt. Kizito
10. Mt. Isidori Mkulima
11. Mt. Denis
12. Mt. Antoni wa Padua
13. Mt. Rita wa Kashia
14. Mt. Yohane Krisostom
15. Mt. Joseph wa Kopertino (wamerejesha UWAKA pekee)

Uchaguzi wa Vyama vya kitume ngazi ya Jumuiya ni kwa UWAKA, WAWATA, VIWAWA, na Wazee na Wastaafu